

2024 UCHAGUZI WA RAISI WA MAREKANI NA SERA YAUHAMIAJI KUBADILIKI

UNACHO HITAJI KUJUA IKIWA HUNA KITAMBULISHO CHA GREEN CARD AU URAIA WA MAREKANI.


IRC imeunda nyenzo kwa ajili ya watu binafsi wenye kesi za uhamiaji nchini marekani. Tuntumai hii itasaidia watu kuelewa Zaidi mchakato wa uhamiaji na haki zao. Hata hivyo, maelezo haya si mbadala wa ushauri wa kisheria kutoka kwa wakili aliyehitimu au mwakilishi aliyeidhinishwa.

Ilisashwa mwisho Novemba 2024

 Uchaguzi wa Rais wa 2024 umelenga sera ya uhamiaji nchini Marekani. Rais wa zamani Donald Trump, ambaye ametangazwa mshindi wa Uchaguzi wa Urais wa Marekani wa 2024, ametoa wito wa kuwepo kwa sera kali za uhamiaji na ongezeko la watu kufukuzwa nchini.

 Kesi ya uhamiaji ya kila mtu ni ya kipekee. Tafadhali zungumza na wakili wa uhamiaji au mwakilishi wa kisheria aliyeidhinishwa na Idara ya Haki kuhusu chaguo yako.

Je, huna uhakika kuhusu jinsi hali yako ya uhamiaji inaweza kuathiriwa na Rais mpya wa Marekani? Hapa kuna baadhi ya majibu na mapendekezo:




HAKUNA MABADILIKO YA HARAKA.

Rais mpya hawesi kufanya mabadiliko yoyote kwenye sera ya uhamiaji hadi baada ya siku ya kuapishwa, Januari 20, 2025 wakati rais mpya atakapokula kiapo.



HALI FULANI ZA UHAMIAJI NI ZA MUDA

Hizi ni pamoja:



- Hali Iliyolindwa kwa Muda (TPS)
- Kitendo Kilichoahirishwa kwa Waliofika Utotoni (DACA)
- Kuondoka Kwa Kulazimishwa Kumeahirishwa (DED)
- msamaha (wakati mwengine huitwa msamaha wa Kibinadamu au msamaha wa Uhamiaji)

The new president of the United States has the power to end these types of temporary statuses. In some cases, this may take a few months or longer. In other cases, the President of the United States can make changes that will affect people immediately. It is impossible to predict when or how immigration policies will change.

JE, UNA GREEN CARD AU URAIA WA MAREKANI?

Ikiwa sivyo, zungumza na wakili wa uhamiaji au mwakilishi aliyeidhinishwa na Idara ya Haki kuhusu chaguo yako ili kupata hadhi ya kudumu ya uhamiaji. Wakili wa uhamiaji au mwakilishi aliyeidhinishwa angalia kama unastahiki hadhi ya kudumu. Iwapo unastahiki hali ya kudumu ya hali ya uhamiaji, unashauriwa kuifuata, bila kujali ni nani aliye Rais wa Marekani.



EPUKA ULAGHAI WA UHAMIA!

Kumbuka kwamba mawakili wa uhamiaji pekee na wawakilishi walioidhinishwa wanaweza kukupa ushauri wa kisheria. Jihadharini na notario au notaries (wapiga muhuri) za kijamii ambaa hawajaidhinishwa au wamehitimu kutoa ushauri wa uhamiaji. Watakupoteza muda na pesa na wanaweza kukuweka wewe na kesi yako kwenye hatari kubwa.



Kabla ya kuajiri mtu kukusaidia kwenye kesi yako, muulize mtaalamu kuhusu sifa zake. Je, mtu huyo ni wakili au mwakilishi aliyeidhinishwa? Je, mtu huyo ana uzoefu kiasi gani kwenye sheria ya uhamiaji? Bonyeza hapa Immigration Scams kwa maelezo zaidi kuhusu Ulaghai wa Uhamiaji. Pia bonyeza hapa this directory ili kupata mtoe huduma wa kisheria aliyeidhinishwa ambae anaweza kukusaidia kwa gharama nafuu au bila malipo.

UKO NA HAKI

Watu wote wanaoishi Marekani wana haki fulani za kimsingi chini ya Katiba ya Marekani. Watu walio na hali ya uhamiaji wa muda wana haki hizi, pia. Jua haki zako na usiogope kuzitumia unapowasili ana polisi au maafisa wa Uhamiaji na walindaji wa mipaka(ICE).

Ikiwa umesimamishwa au kuhojiwa na polisi au na afisa wa uhamiaji,

kumbuka kwamba una haki zifuatazo:

- Ikiwa wewe si raia wa Marekani na afisa wa uhamiaji anaomba karatasi zako, lazima uzionyeshe ikiwa unazo. Ikiwa una zaidi ya miaka 18, beba hati zako za uhamiaji kila wakati. Ikiwa huna karatasi za uhamiaji, sema unataka kukaa kimya.
- Unaweza kukataa kuzungumza nao. Si lazima ueleze ulikozaliwa au jinsi ulivyoingia Marekani.



- Una haki ya kuzungumza na wakili.
- Kabla ya kusaini chochote, zungumza na wakili.
- Kuwa na kadi ya maelezo ya Haki Zako na uionyeshe ikiwa afisa wa uhamiaji atakusimamisha (tafuta kadi hapa katika lugha yako).

Je, unahitaji maelezo zaidi au usaidizi?



IMtandao wa Mawakili wa Uhamiaji

kwa vijana walioingia Marekani bila mzazi au mlezi halali:



ImportaMi

